

OFISI YA RAIS -TAMISEMI

SHULE YA SEKONDARI UKWAMA,

S. L. P 145,

Kumb. Namb.....

MAKETE.

Tarehe.....

JINA LA MWANAFUNZI

S.L. P

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA, SHULE YA SEKONDARI MWAKA 2021

1. Nina furaha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii, mwaka 2021. Shule ya sekondari Ukwama ipo umbali wa km 43 toka halmashauri ya wilaya ya Makete. Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe 11/01/2021 unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 15/01/2021
2. Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1. Sare ya shule ni

- i. Mashati mawili meupe ya tetroni ya mikono mirefu kwa wote yawe ya mshono wa kawaida na mfuko mmoja.
- ii. Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili vyenye kisigino kifupi vya kufunga kwa gidamu kwa wote .
- iii. Soksi jozi tatu , wasichana rangi nyeupe na wavulana rangi nyeusi.
- iv. Sweta moja rangi ya damu ya mzee na moja rangi ya kijivu aje nayo. (Makoti na jaketi hayaruhusiwi.)
- v. Kila mwanafunzi anapaswa kuwa na mavazi ya michezo. (Raba pea moja, track full suit rangi ya bluu)
- vi. Suruali moja ya rangi ya dark blue na moja rangi ya kijivu aje nazo kwa wavulana.
- Vii. Sketi moja ya rangi ya dark blue na moja rangi ya kijivu na suruali moja rangi ya dark blue na moja rangi ya kijivu watakazo vaa kwa pamoja.

2.2. Daftari, kalamu na mkebe wa hesabu na rimu moja ya kufanyia mazoezi yake.

2.3. Vifaa vya usafi wake binafsi fagio aina ya chelewa, ndoo ya lita 10, Jembe na mpini.

2.3. Kwa kuwa shule ni ya kutwa gharama za chakula ni jukumu la mzazi /mlezi

- a) Mchango wa chakula ni mahindi madebe manne b) Maharage debe moja, c) Mchele lita kumi d) Fedha Tsh 55,000/- kwa muhula.

3.1. Sheria na kanuni muhimu za shule.

- a. Heshima kwa viongozi, wazazi, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- b. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli za ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- c. Kushiriki kwa makini kufanya maandalizi ya jioni (preparation).
- d. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule.
- f. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- g. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- h. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
- i. Kutunza mali za shule.

3.2. Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule

- a. Wizi.
- b. Uasherati na ushoga.
- c. Ubakaji.
- d. Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya kama vile uvutaji wa bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
- e. Kupiga au kupigana.
- f. Kuharibu kwa makusudi mali za umma.
- g. Kudharau Bendera ya Taifa.
- h. Kuoja au kuolewa.
- i. Kutoa mimba.
- j. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki katika uvunjifu wa amani na usalama wa shule au watu.
- k. Kukataa adhabu kwa makusudi.
- l. Kuwa na simu ya mkononi.

OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI

SHULE YA SECONDARI UKWAMA

A. HABARI BINAFSI ZA MWANAFUNZI

1. Jina Kamili
2. Tarehe ya kuzaliwaWilaya
3. Jina la baba mzazi kabila
4. Anayegharamia elimu ya kijana ni
Uhusiano wake na mwanafunzi ni
Kazi afanyayo ni
5. Anwani ya anayeishi na mwanafunzi niSimu namba
.....

B. TAMKO LA MZAZI/ MLEZI

Mimi nakubali mwanangu asome katika shule hii na naahidi kumtimizia mahitaji yote yanayotakiwa ikiwa pamoja kumnunulia sare ya shule kwa wakati na kushirikiana na uongozi wa shule katika kuboresha masomo na mwenendo wa tabia nzuri ya mwanafunzi huyu.

C. REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

To medical officer

MAKETE Government hospital

Please examine the above named youth as to her /his fitness pursue secondary school classes as well as conduct manual activities as a day school student.

D. MEDICAL OFFICER(S) RECOMMENDATION

..... has examined the above mentioned student and has found him / her fit / unfit to pursue studies at secondary school level.

I recommend as overleaf for improvement.

Name Signature..... Date.....

.....

JOHN M. SAADAN

MKUU WA SHULE